*Mulika, Juz. 44(2), 268-290*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Usawiri wa Wahusika wa Ajabuajabu katika Riwaya Teule za Kihalisiajabu za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi

*Charles Nyanduru Maggati*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.7

**Ikisiri**

Wahakiki na wataalamu mbalimbali wa kazi za fasihi wamejadili kwa mapana usawiri wa wahusika wa ajabuajabu. Miongoni mwao, kuna wanaobainisha jinsi wanavyojitokeza katika kazi za fasihi, namna wanavyoweza kuakisi uhalisia wa maisha katika jamii na kile kilichokusudiwa na mtunzi katika kuwatumia. Pamoja na kazi hizo kuchangia katika kuelewa kazi za fasihi zinazotumia wahusika wa ajabuajabu, aina za wahusika wa ajabuajabu hazijajadiliwa kwa kuzingatia upekee na umuhimu wake. Makala hii inabainisha aina za wahusika wa ajabuajabu kama zinavyojitokeza katika riwaya za Kiswahili za kihalisiajabu kwa kuangazia riwaya za *Kusadikika* (1951) na *Adili na Nduguze* (1952) za Shaaban Robert na *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991) za Euphrase Kezilahabi. Riwaya hizo ziliteuliwa baada ya kusoma riwaya mbalimbali zenye wahusika wa ajabuajabu na kubaini kuwa ndizo zenye data toshelevu zinazosadifu mahitaji ya makala hii. Data zilikusanywa kutoka vitabu teule kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Uchambuzi na uwasilishaji wa data katika makala hii umeongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu ya Franz Roh (1925) kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Nadharia hii imewezesha pia kuwabainisha wahusika wa ajabuajabu katika riwaya teule. Kwa kuzingatia kigezo cha kimaana, imebainishwa kuwa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia aina za wahusika wa ajabuajabu kusawiri hali na matukio halisi katika jamii zao.

## 1.0 Utangulizi

Wataalamu kadhaa wa fasihi wanaeleza maana ya wahusika kwa namna mbalimbali. Rono (2013) anaeleza kuwa wahusika ni viumbe wanaosawiriwa kisanaa na mwandishi kwa makusudi ya kuwakilisha dhana, mawazo au tabia za watu katika kazi ya fasihi. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi ambao wanafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Ni viumbe ambao hutumiwa na mwandishi katika mtiririko wa matukio kuelezea kisa chake. Wanatumiwa na msanii kusimamia hali mbalimbali za binadamu katika jamii wanamoishi. Wahusika ndio wanaotumiwa na msanii kutoa picha au kuwakilisha mawazo na fikra au maudhui yake kwa jamii inayowakilishwa na wahusika hao.

[1] Mhadhiri, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania, Baruapepe: nyandurucharles@gmail.com/charles.maggati@muce.ac.tz

Wahusika wanaweza kuwa watu, majitu, miti, wadudu, mizimu, misitu, wanyama, mawe na hata mashetani (Madumulla, 2009; Senkoro, 2011). Hivyo, wahusika katika kazi za fasihi huumbwa ili kujenga mori ya aina fulani katika hisia za hadhira. Ni wawakilishi wa tabia, matendo, hulka na silka kulingana na muktadha au mazingira fulani maalumu yanayoafikiana na mila na desturi za jamii husika. Kwa mfano, wahusika kama sungura hutumiwa kuhadaa hadhira, simba kutishia, mazimwi kuogofya wakati fisi hutumiwa kuchekesha hadhira kwa tabia zao za uroho, ulafi, uzembe na ujinga.

Wahusika ndio nguzo kuu ya dhamira na maudhui katika kazi ya fasihi. Hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili kuwakilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii husika. Ili kufahamu aina za wahusika katika kazi ya fasihi ni muhimu kuangalia: majina waliyopewa, maneno yao, mwandishi anasema nini kuhusu wao, wanatenda nini, wahusika wengine wanawasemaje na wana jukumu na umuhimu gani katika kazi husika (Wamitila, 2010).

Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida (Wamitila, 2003). Kinyume na kazi zenye kufuata mkondo wa uhalisia, kazi zinazoegemea mkondo wa uhalisiajabu zinamsawiri mhusika kwa namna isiyokaribiana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida.

Bosibori (2016) anaeleza kuwa mhusika ni mtendaji katika kazi ya fasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na sifa za binadamu. Mhusika katika mkondo wa uhalisiajabu anaweza kufanya mambo ambayo hayawezi kufanywa na binadamu katika ukawaida wake. Wahusika hawa wanaweza kujitokeza katika sura tofautitofauti zinazotofautiana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida ndani ya kazi moja ya kifasihi. Kwa mfano, mhusika anaweza kujitokeza kama jini, malaika, mnyama au ndege na pia kuingia pasipoingilika na kula au kumeza yasiyomezeka katika uhalisia.

Mturo (2018) anatumia neno wahusika wa kinjozi anapowaelezea wahusika wa ajabuajabu. Anasema kwamba wahusika hawa hutumiwa kueleza na kuwasilisha fikra na uwazaji wa kiwango cha juu na matukio yasiyokuwa ya kawaida. Usawiri wa wahusika wa kinjozi ni mpana mno na huweza kujumuisha bunilizi za kisayansi na kazi za kihalisiajabu zinahusishwa na matukio yasiyokuwa ya kawaida. Kwa mfano, ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Pia, viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizimu, majitu, majini pamoja na wanyama hurejelewa.

Onchwati (2016) anasema kuwa wahusika wanakuwa wa ajabuajabu pale wanapotenda au kujitokeza katika hali inayokiuka uhalisia au uasilia wa maumbile au uwezo wa binadamu wa kawaida katika maisha halisi. Makala hii, kwa kutumia riwaya teule za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi, inabainisha aina za wahusika wa ajabuajabu kutokana na namna walivyosawiriwa katika riwaya teule.

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya Teule

Ili kuwa na uelewa wa pamoja baina ya mwandishi na msomaji, inafaa kutoa muhtasari wa riwaya teule zilizotumiwa katika makala hii. Riwaya hizo ni *Kusadikika*, *Adili na Nduguze na Nagona* na *Mzingile.*

### 2.1 *Kusadikika*

Ni riwaya iliyotungwa na Shaaban Robert na kuchapishwa mwaka 1951. Riwaya hii inaanza na tukio la kushtakiwa kwa mhusika mkuu, Karama, kwa tuhuma za kuihujumu Serikali ya Kusadikika. Hujuma hizo zinatokana na Karama kutoa elimu ya sheria ambayo ingewafanya wananchi kufahamu haki zao na, hivyo, kutoitii serikali yao. Karama alithibitisha mbele ya Mahakama ya Kusadikika jinsi serikali ilivyoshindwa kuthamini michango ya raia wake kwa kuelezea historia ya wajumbe sita waliotumwa nchi mbalimbali kwenda kufanya utafiti wa jinsi ya kuendeleza nchi yao. Katika safari za wajumbe hao sita, matukio ya ajabu na wahusika wa ajabuajabu wanajitokeza. Wahusika hao wa ajabuajabu ni pamoja na wale wanaoweza kula tani milioni za chuma, kunywa maji yote ya mto na kumeza tani nyingi za magogo bila kushiba. Kuna uvunjivu wa kaida za mawasiliano ambapo binadamu wanazungumza na malaika na mashetani. Hakuna kizuizi cha umbali wala mazingira ambapo mtu anaweza kusafiri hadi mbinguni na kuingia ndani kabisa ardhini bila pingamizi lolote kwa kujifunga katika miguu ya ‘Mangera’ (aina ya ndege wakubwa sana wanaoishi Kusadikika ambao hujitafutia malisho yao katika ardhi). Kuna wahusika wenye uwezo wa kusema neno tu na mtu akawa kipofu bila kupakwa dawa yoyote wala kuguswa kwa mkono.

### 2.2 *Adili na Nduguze*

Hii ni riwaya iliyotungwa na Shaaban Robert na kuchapishwa mwaka 1952. Robert, katika *Adili na Nduguze*, anashughulikia mambo mengi yahusuyo tabia mbalimbali za watu. Anasisitiza kuwa uovu hushindwa kwa kutenda wema, yaani wema ni akiba. Adili alimwokoa Huria alipokaribia kuuawa na Hunde. Huria naye alilipa fadhila hiyo kwa kumwokoa Adili alipotoswa baharini na ndugu zake, yaani Hasidi na Mwivu. Robert, katika riwaya hii, anawasawiri wahusika wa ajabuajabu wanaofanya matukio ya ajabuajabu yanayovunja kaida za uhalisia na uasilia. Kuna majini yanayozungumza na wanadamu, yanayobadilika sura mbalimbali, yanayoweza kumbadilisha binadamu

kuwa nyani na yanayoweza kuingia popote hata chini ya ardhi bila kizuizi chochote. Wahusika hawa wana uwezo wa kuhisi, kuona na kufahamu mambo yanayotendwa mbali na mahali walipo, kufika na kuingia popote bila kizuizi cha umbali wala mazingira. Wahusika wengine ni warefu kiasi cha kuvuka bahari bila maji kufika magotini. Wepesi kiasi cha kuzunguka dunia nzima kwa dakika tano na wenye nguvu kiasi cha kumkamata nyangumi baharini na kumwoka kwa jua angani. Wahusika wengine wana uwezo wa kusema miji ikagharikishwa na watu pamoja na vitu vyote kugeuka mawe.

### 2.3 *Nagona*

Ni riwaya iliyoandikwa na Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1990. Hii ni riwaya ya kifalsafa iliyoandikwa kwa kutumia mbinu ya uhalisiajabu ikichambua masuala mbalimbali yahusuyo maisha. Mhusika mkuu, 'Mimi', anakutana na mazingaombwe mengi ya kutisha akiwa katika safari ya kutafuta jibu la maana ya maisha. Kezilahabi, katika riwaya ya *Nagona,* anawasawiri wahusika wa ajabuajabu wanaofanya matukio ya ajabuajabu yanayovunja kaida za uhalisia na uasilia. Kuna wahusika wanaoweza kubeba na kuhamisha milima, wanaoweza kunywa maji yote ya mto na kuyatapika ili kulowanisha ardhi kavu. Wahusika wenye uwezo wa kubeba mimba miaka milioni na bado mtoto akazaliwa kabla ya siku zake. Kuna wahusika wenye nafsi mbili, wenye uwezo wa kufa na kuishi kwa wakati huohuo na kujibadilisha sura mbalimbali. Kuna wafu wanaoongea na walio hai, wenye uwezo wa kufufuka, kutapika, kuzungumza na kusafisha roho zao na roho zao kupotea lakini wakaendelea kuishi. Vilevile, Kezilahabi amewachora wahusika wenye uwezo wa kukunja na kukunjua mguu kufuata kitu kilicho umbali wa kilomita nyingi kwa muda mfupi. Wahusika wengine wana uwezo wa kufahamu anayoyawaza mtu na miili inayotoa mwanga. Pia, kuna matukio yanayotendwa na watu wasioonekana, maiti kubeba *Biblia* na *Kurani*, Paa anayebadilika katika sura mbalimbali pamoja na miti na misitu inayoongea.

### 2.4 *Mzingile*

Riwaya hii imetungwa na Euphrase Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1991. Riwaya inaanza na kisasili cha kuzaliwa mtoto-kizee anayeanza kuongea akiwa tumboni. Riwaya hii inahusu motifu ya safari ya shujaa anayejiita 'Mimi'. Mimi anatumwa kupeleka taarifa za kifo cha Mkombozi wa pili kwa baba yake anayeitwa 'Mzee'. Safari hiyo inampeleka pia katika kutafuta kiini na maana ya maisha. Mimi anafanikiwa kumpata Mzee anayeishi katika kijumba chake juu ya mlima na kufanya naye mazungumzo. Hata hivyo, Mimi anashindwa kumshawishi Mzee kuhudhuria mazishi ya mwanawe. Kutokana na hali hiyo, Mimi anaamua kurudi na safari yake inampeleka katika kutafuta majibu ya maswali ambayo hakuulizwa. Inamchukua

Mimi karne nyingi kufika kijijini kwake. Anapofika, anagundua kuwa kijiji kimeharibiwa na mabomu ya nyuklia na kubaki magofu.

Anapoingia katika nyumba yake iliyoharibiwa, Mimi anamkuta Mzee na mazungumzo yanaendelea. Baada ya muda, mvua inaanza kunyesha na uoto unarudi katika hali yake. Katika kipindi hiki ‘mwanamke’ anajitokeza kimaajabu na kumwongoza Mimi kuelekea ulimwengu mpya na kumwacha Mzee ambaye baadaye anatoweka. Mimi na mwanamke wanaishi pamoja na kuanzisha ulimwengu mpya. Wote wanaonekana kujua makosa yaliyofanyika zamani. Ili kuepukana na makosa hayo hapo baadaye, wanaamua kujenga ulimwengu mpya bila kutumia maarifa yaliyopo.

Kezilahabi, katika riwaya ya *Mzingile*, anawasawiri wahusika wa ajabuajabu wanaofanya matukio ya ajabu yanayovunja kaida za uhalisia na uasilia. Kuna wahusika wanaoweza kujibadilisha kimazingaombwe, wanaoweza kufa na kuishi kwa wakati mmoja, wanaoweza kutoweka kimiujiza na wenye miili inayotoa mwanga. Wahusika wengine wana uwezo wa kuongea wakiwa tumboni, wanaofahamu anayoyawaza mtu. Pia, kuna matukio yanayotendwa na watu wasioonekana pamoja na wanyama wanaoweza kuongea na wanadamu.

**3.0 Misingi ya Kinadharia**

Mtindo na msingi wa uhalisiajabu katika fasihi ilikuwa ya awali zaidi, hasa katika kaida za kiramsa ambapo masimulizi yaliyaweka sambamba matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida (Green, 2009). Warner (2006) anaeleza kuwa matumizi ya awali kabisa ya istilahi ‘uhalisiajabu’ yalianza kutumika katika maandiko ya mshairi Fredrich Freiherr von Hardenberg aliyejulikana kwa lakabu ya kishairi, ‘Novalis’. Hata hivyo, wahakiki kama vile Abrams (1999) na D’Haen (2005) wanadai kuwa uhalisiajabu, kama dhana au istilahi, umeanza kutumika kunako miaka ya 1920 na kuungana na Schroeder (2004) anayedai kwamba mchoraji na mpigapicha wa Kijerumani, Franz Roh, ndiye aliyevumbua matumizi ya uhalisiajabu mwaka 1925 katika kazi yake kuhusu mtindo wa sanaa ya kisasa ya Ulaya ya wakati huo. Hii ni kwa sababu Roh ndiye aliyetumia kwa mapana istilahi ya uhalisiajabu kuliko wengine wote waliomtangulia na kuhesabiwa kuwa mwasisi wa nadharia hii. Roh aliutambulisha uhalisiajabu kama picha au sanamu iliyotengenezwa kwa uwazi wa pekee kusawiri uasilia wa uhalisiajabu katika ulimwengu halisi na wakati huohuo ikitafsiri uajabu wa watu katika ulimwengu wa sayansi na ufundi au teknolojia ya kisasa.

D'Haen (2005) anaeleza kuwa Roh alilibuni neno hili kuelezea michoro iliyo na uhalisia kama wa picha ya kamera lakini iliyoibua hisia za kutokuwa halisi kwa kuchanganya uhalisia na ukosefu wa uhalisia. Baadaye uhalisiajabu ulitumiwa kuelezea mambo ya ajabuajabu yanayosawiri uhalisia na wachoraji wa Amerika Kusini kama vile Ivan Albright, Paulo Cadmus na George Tooker kati ya miaka ya 1940 na 1950 (Maggati, 2022). Miongoni mwa waandishi wa fasihi waliovutiwa na sanaa hii ya uchoraji wa Wajerumani ni pamoja na Massimo Bentempelli wa Italia, Hubert Lampo wa Ubelgiji na Arturo Uslar-Pietri wa Venezuela. Leal (2009) anasema kuwa Pietri ni miongoni mwa walioanza kutumia istilahi *realismo magico*, yaani 'uhalisiajabu katika fasihi' mwaka 1948.

Zamora na Faris (2005) wanasema kwamba uhalisiajabu unaafiki kutalii na kukaidi mipaka, si hoja kama mipaka hiyo ni ya kiontolojia, kisiasa, kijiografia au ya kiutanzu. Uhalisiajabu, unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama nadharia inayowakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha (Walibora, 2010).

Mbatiah (2002) anaeleza kwamba istilahi hii inatumiwa kueleza mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia, yaani kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wamitila (2008) anamuunga mkono Mbatiah kwa kudai kuwa dhana ya uhalisiajabu huhusishwa na Amerika ya Kusini au hata nchi zinazoitwa za ulimwengu wa tatu. Sifa yake kuu ni kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabuajabu na ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa maana inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika. Katika nadharia hii, hali za kushangaza na kuogofya, huwasilishwa kana kwamba ni hali za kawaida. Wasomaji, wasikilizaji na watazamaji huelezwa mambo ya kiajabuajabu na kuaminishwa kuwa hayo mambo ni ya kawaida na yanaweza kutokea katika ulimwengu wanamoishi. Mambo yanayoelezwa ni ya ajabu ama ya kichawi ambayo ni sehemu ya mwonoulimwengu wa jamii husika.

Bowes (2004) anasisitiza kuwa uhalisiajabu hutumika kuelezea mambo ya kweli, halisi, yanayoonekana na kugusika na wakati huohuo huingiza ushetani, umizimu na mazingaombwe katika mazingira halisi kutegemeana na utamaduni wa jamii husika. Uhalisiajabu ni nadharia ya fasihi inayokutanisha uhalisi na mambo ya ajabu au ya kuogofya ambayo si ya kiuhalisia wa kawaida unaofahamika. Ni mbinu ya kuangalia mambo ya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida ambapo msomaji na mwandishi

wanaamini kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya ulimwengu wa sanaa na ulimwengu wao wa kawaida wanapoishi (Maggati, 2022).

Nadharia ya Uhalisiajabu imetumiwa katika makala hii kwa sababu mihimili yake inatosheleza kusawiri na kubainisha wahusika wa ajabuajabu wanaopatikana katika riwaya teule. Mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu iliyotumiwa katika makala hii ni, kwanza, katika uhalisiajabu kaida za uhalisia na uasilia huvunjwa; hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha au kumbadilisha mtu mwingine sura na kuwa kitu kingine. Uhalisiajabu huvunja mpaka kati ya mbali na karibu, uhai na kifo, kweli na uongo na ndoto na uhalisia. Kwa hiyo, mtu anaweza kusafiri na kufika mbali sana, mathalani, mbinguni, kwa dakika moja au kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Pili, kaida za kimazingira na mahali huvunjwa. Hivyo, mtu anaweza kuingia popote hata ndani ya ardhi bila kizuizi, kufahamu yanayotendeka mbali na kufahamu mawazo ya mtu pamoja na kuzungumza na viumbe wengine bila kizuizi cha tofauti ya lugha. Hii ni kwa sababu, katika uhalisiajabu, hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi. Tatu, uhalisiajabu haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, ugeni na wenyeji na tamaduni zinaingiliana. Katika uhalisiajabu, viumbe wa ajabuajabu wenye nguvu na uwezo wa ajabu kama mazimwi, majitu makubwa, mashetani, mizuka, majini, wanyama pamoja na misitu mikubwa, mito na bahari hurejelewa.

### 4.0 Aina za Wahusika wa Ajabuajabu katika Riwaya Teule

Wataalamu wa fasihi hutumia mbinu tofautitofauti katika kubainisha aina za wahusika. Mbinu hizo ni pamoja na majina waliyopewa, maneno yao, mwandishi anasema nini kuhusu wahusika, wanatenda nini, wahusika wengine wanawasemaje, wana kazi gani au jukumu gani katika kazi husika; wana mtazamo gani, wana umuhimu gani, kukubalika kwao kama wahusika wa kifasihi na usahali na uchangamano wao. Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa mbinu hizo, hakuna mbinu iliyo kamilifu inayoweza kutumika kubainisha aina za wahusika wa ajabuajabu kwa kadiri wanavyojitokeza. Wamitila (2010) anasisitiza hoja hiyo anaposema kuwa kazi ya fasihi hutegemea zaidi msanii anayehusika katika uibuaji wa aina mbalimbali za wahusika. Aidha, ili kubaini aina za wahusika wa ajabuajabu miongoni mwa mbinu tajwa, makala hii kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Uhalisiajabu, imezingatia kwa pamoja: maneno ya wahusika, mwandishi anasema nini kuhusu wahusika, wanatenda nini na jinsi wahusika wengine wanavyowasema. Mbinu hizo zimewezesha kubainishwa kwa aina tano za wahusika wa ajabuajabu kutoka riwaya teule: wahusika wenye uwezo wa kujibadilisha kimazingaombwe, wahusika majitu wenye uwezo na nguvu za ajabu, wahusika wenye uwezo wa kufahamu mawazo ya

mtu, wahusika hai-wafu, na wahusika wenye uwezo wa kuvunja kaida za mawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine.

### 4.1 Wahusika wenye Uwezo wa Kujibadilisha Kimazingaombwe

Osore (2008) anaelezea kujibadilisha kimazingaombwe kama mabadiliko ya matukio na wahusika yanayohusishwa na ukiushi wa kimaumbile kutoka hali fulani ya maisha au uwapo kwenda hali nyingine. Kujibadilisha kimazingaombwe ni fumbo au muujiza wa kushtukiza unaoshangaza na wa kutatanisha. Ukweli wake kukubalika katika maisha halisi na ya kila siku kwa akili ya kawaida kunabaki kuwa ni swali ambalo kiini cha jibu lake kinabakia kuwa kisasili. Ni jambo lisiloweza kuelezeka wala kufumbuliwa kisayansi au kwa kutumia mantiki au akili ya kawaida ya binadamu bali kwa kutumia uhalisiajabu. Lengo mojawapo la kutumia mbinu hii ni kuelezea mambo ya kawaida kwa njia isiyo ya kawaida.

Kujibadilisha kimazingaombwe ni aina fulani ya uhalisiajabu inayomwezesha mtumiaji wa mbinu hiyo kujibadilisha na kuwa mtu mwingine au kitu kingine. Mtumiaji anaweza kujigeuza kiumri, umbo, na hata jinsi; anaweza kutumia miujiza au mbinu mbalimbali za kifantasia, ikiwa ni pamoja na kujibadilisha kuwa ng'ombe, nyoka, mizimu, mti wa mrumba au mpingo. Pia kubadili vitu mbalimbali katika maumbo tofauti au kuwa vitu vingine tofauti kabisa (Mpalanzi, 2018).

Jinsi wahusika wanavyojibadilisha au kuwabidilisha wahusika wengine kuwa viumbe wengine inadhihirishwa na mhimili wa uhalisiajabu unaosisitiza kuwa, katika uhalisiajabu, kaida za uasilia na uhalisia huvunjwa. Hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha au kumbadilisha mtu mwingine sura na kuwa kitu kingine. Robert na Kezilahabi wamebainisha aina hii ya wahusika kwa kuzingatia matendo yao, maneno yao, jinsi wahusika wengine wanavyowasema na mwandishi anasema nini kuhusu wahusika. Shabaan Robert anathibitisha hili kwa kumtumia Huria binti Kisasi.

Huria anajibadilisha kuwa viumbe mbalimbali ili kujiokoa au kumkwepa jini, Hunde Waziri wa Ngazi, aliyetaka kumuua kwa sababu Huria alikataa posa yake. Kwa kuogopa kushambuliwa na Hunde, Huria alijibadilisha sura kila alipotoka kutembea. Hata hivyo, kila Huria alipojibadilisha, Hunde naye alijibadilisha na kunusa harufu ya Huria kama mbwa. Huria alipojigeuza panya, Hunde alijigeuza paka; akiwa paka, yeye anakuwa chui; akiwa chui, Hunde anajigeuza simba. Siku aliyojigeuza tandu, yeye alikuwa nyoka akamfuata (Robert, 1952).

Huria anajibadilisha pia kuwa ndege wa kutisha ili kumwokoa Adili baharini alipotupwa na ndugu zake ili kulipa fadhila ya wokovu aliyofanyiwa na Adili

alipotaka kuuawa na jini, Hunde Waziri wa Ngazi. Huria anajibadilisha sura za ajabu kila dakika moja ili kuonesha uwezo wake walipotua kwa ghafla jahazini na Adili kwa lengo la kuwaadhibu Hasidi na Mwivu, ndugu zake Adili. Watu wote jahazini walishikwa na mshangao mkubwa kwa mabadiliko yake ya mfululizo, wakatosheka kuwa aliweza kubadili kitu chochote katika umbo alilotaka (Robert, 1952).

Robert ametumia kujibadilisha kwa Huria kuwa viumbe mbalimbali, katika azma ya kumkwepa Hunde, kuelezea katika uhalisia uchafu, uchoyo na ukandamizaji unaofanywa na wanaume wasioadilika wanaotumia nguvu, vyeo na uwezo wao kifedha kutaka kuwaoa wanawake. Amewatumia Huria binti Kisasi na jini, Hunde Waziri wa Ngazi, aliyetaka kumwoa Huria kwa nguvu kama mfano kuelezea uovu, uchafu na ubinafsi wa wanaume, ufisadi unapowapofusha.

Salim (2015) anaeleza kuwa Robert amemtumia nyoka, yaani Hunde Waziri wa Ngazi, kuwakilisha nchi tajiri ulimwenguni ambazo hutumia nguvu zake ili kukandamiza, kuonea, kunyanyasa na kunyonya nchi maskini. Pia, amemtumia tandu kuwakilisha nchi changa zinazokandamizwa.

Robert amemtumia pia Huria kujibadilisha ndege wa kutisha ili kumwokoa Adili katika hatari ya kufa maji na, hivyo, kufanikisha azma yake ya kulipa fadhila na ahadi aliyotoa kwa Adili kueleza kuwa wema hauozi. Adili alimwokoa Huria mikononi mwa Hunde na sasa Huria naye amemwokoa Adili asizame baharini. Mwandishi anasisitiza kuwa wema asilia ni mzuri zaidi na una thamani kubwa. Deni la wema haliwezi kulipwa milele hata kama itatumika gharama kubwa kiasi gani. Kwa kusisitiza hili anasema:

> Adili alijibu: “Deni langu limekwisha lipwa lote. Niliokoa maisha ya binti yako naye ameokoa yangu. Hapana deni tena kati yetu”. Malkia wa majini alitabasamu akasema: “Wema wako ulikuwa asilia, nawe ulitangulia kuutenda; wa binti yangu ulikuwa wa kuigiza, naye ameutenda nyuma. Asili na uigaji ni vitu mbalimbali. Havilinganiki wala havitalinganika milele” (Robert,1952:36).

Robert anamtumia Huria kujibadilisha sura za ajabuajabu na za kutisha wakati alipokuwa akitoa adhabu ya kuwabadilisha Hasidi na Mwivu manyani kudhihirisha uhalisia kwamba haifai kuwa na mzaha katika kukemea au kuwaadhibu waovu. Hivyo, yeyote mwenye tabia chafu kama ya Hasidi na Mwivu anastahili kuadhibiwa bila huruma. Pia, anamtumia Huria kuwabadilisha Hasidi na Mwivu kuwa manyani kusisitiza kuwa kila tendo baya linastahili kuadhibiwa bila kujali kuwa mkosaji ni

nani. Sheria zisibadilishwe wala kutungwa kwa kulenga kundi fulani la watu katika jamii bali ziwe kwa ajili ya wote na kwa maslahi ya jamii nzima.

Kezilahabi naye anatumia matendo ya wahusika na maelezo ya msimuliaji ambaye anajitambulisha kama Mimi ili kupata wahusika wanaojibadilisha kimazingaombwe. Kezilahabi anamtumia mhusika Paa anayejibadilisha na kujidhihirisha kwa sura tofautitofauti. Paa anajitokeza kama mnyama ambaye anafuatiliwa nyayo zake. Pia, anajitokeza kama kiumbe aliyefunikwa gubigubi mwenye uwezo wa kucheza bao na wanadamu. Vilevile, Paa anajitokeza kama msichana mrembo ambapo msimuliaji msaka Paa anamwita binti. Aidha, anajitokeza kama kiumbe wa ajabu mwenye mwili unaotoa mwanga. Kadhalika, Paa anajitokeza kama kitu kizito kinachomkalia msimuliaji mabegani. Msimuliaji anathibitisha kwa kusema kwamba Paa ana uwezo wa kujibadilisha kimazingaombwe na kujitokeza kama mnyama, kama msichana mzuri, kama kiumbe chenye kutoa mwanga, chenye uwezo wa kuruka milima na kama kitu kisichojulikana (Kezilahabi, 1990).

Kezilahabi anambainisha pia Nagona kama aina ya mhusika anayejibadilisha kimazingaombwe. Nagona anajitokeza kwa sura na namna tofautitofauti. Anajitokeza kama mwanga, kama mtoto mdogo wa kike anayezaliwa kabla ya siku zake ingawa mimba yake ni ya mamilioni ya miaka. Anajitokeza kama jua lililopatwa na mwezi na pia kama mkombozi wa pili.

Kujibadilisha kwa Paa na Nagona katika sura mbalimbali ndiko kunakofanya waainishwe kama wahusika wa ajabuajabu. Hii ni kwa sababu kubadilikabadilika huko hakuwezi kuelezwa wala kufumbuliwa kwa kutumia nadharia za kisayansi au kaida za kijadi zenye mwono mmoja tu wa uhalisia. Hii inathibitishwa na mhimili wa uhalisiajabu unaosema kuwa, katika uhalisiajabu, kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa; hivyo, binadamu anaweza kujibadilisha sura na kuwa kitu kingine (Roh, 1925).

Kezilahabi, kwa kuwasawiri wahusika wanaobadilika kimazingaombwe—Paa na Nagona—, anakusudia kuzungumzia mambo mawili: kufikiri kwa makini na kweli. Anasema kwamba Babu alipoulizwa na mjukuu wake kuwa Nagona ni nini, alijibu kuwa mtu yeyote mwenye uwezo wa kufikiri amepata kumjua. Alipokuwa mvivu wa kufikiri, Nagona alimpotea kabisa na alipofikiri kwa makini, alimtokea tena. Anaendelea kusema kwamba Nagona anaonekana kama mtu, atajituliza na kufikiri zaidi na kuona zaidi ya fikra. Nagona ni mwanga. Alipo, uongo umejitenga (Kezilahabi, 1990).

**4.2 Wahusika Majitu wenye Uwezo na Nguvu za Ajabu**
Katika sehemu hii, wamesawiriwa wahusika wenye nguvu za ajabu wanaoweza kubeba viumbe wakubwa kama nyangumi; wanaoweza kubeba na kuhamisha milima, kunywa maji yote ya mto na kufuata kitu kilicho mbali sana kwa kukunjua mguu.

Ili kubainisha wahusika majitu wenye uwezo na nguvu za ajabu, tumetumia mhimili wa uhalisiajabu unaosema kuwa, katika uhalisiajabu, viumbe wa ajabuajabu wenye uwezo na nguvu kupindukia kama mazimwi, majitu makubwa, mashetani, mizuka, majini, wanyama pamoja na misitu mikubwa, mito na bahari hurejelewa. Robert anatumia aina hii ya wahusika anapomwelezea Mrefu, jitu refu la ajabu, lenye uwezo na nguvu kupindukia, anaposema:

> Mrefu alikuwa mwujiza katika viumbe. Alikuwa na miguu mikubwa na mapaja manene, kiuno cha utambo na kifua kipana; na shingo yake ndefu ilichukua kichwa kikubwa. Mabega yake ya mraba yalining'iniza chini mikono iliyokuwa na nguvu kama manjanika. Kwa kimo cha kukithiri alitembea baharini bila ya kuguswa na maji magotini, akafikia vilele vya milima kwa mikono yake. Aliweza kukamata ndovu chini au nyangumi baharini akamwoka kwa jua mbinguni. Sauti yake ilikuwa kama radi. Kwa wepesi wake wa ajabu wa kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja, alionekana kama kiumbe kilichoumbwa maalum kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine (Robert, 1952:27).

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa Mrefu si mhusika wa kawaida. Hii ni kwa sababu ni muujiza kumpata binadamu wa kawaida anayeweza kufanana na Mrefu na kufanya anayoyafanya. Mrefu anaweza kutembea baharini bila maji kumfika magotini, mikono yake ni mirefu kiasi cha kufikia vilele vya milima. Ana uwezo wa kumkamata nyangumi au ndovu na kumwoka kwa jua mbinguni. Si hivyo tu, bali pia Mrefu ana sauti kama radi na ni mwepesi kiasi cha kuzunguka dunia nzima kwa sekunde moja (Robert, 1952).

Kinachoshangaza ni kuwa, Mrefu, mbali na uajabu wake, kutisha kwake, uwezo wake, nguvu zake, na kuwa muujiza katika viumbe, lakini Tukufu, mfalme wa mji uliogeuzwa mawe, hakuonekana kutishwa wala kutilia maanani maneno ya Mrefu. Mrefu anamtahadharisha Tukufu kuwa mfalme ni naibu wa Mungu duniani na, kwa sababu ya amana kubwa aliyopewa, anatakiwa kuwa mwadilifu katika matendo yake na kuachana na ibada ya mizimu. Mrefu anasisitiza kuwa, kwa sababu ya uzima wa milele, ibada ya mizimu ni maangamizi na ni ujinga mtupu (Robert, 1952).

Mbali na Tukufu, mfalme wa Fahari, mji uliogeuzwa mawe, kukataa maonyo ya bure kutoka kwa Mrefu, naye anashadidia kuwa Mrefu, kwa sababu ya urefu wake unaomfanya akaribie jua, inawezekana jua limeunguza ubongo wake na hivyo kuharibu akili yake (Robert, 1952). Pia, kwa uwezo wa Mrefu kuokoa kitu hatarini na kwa wepesi wake wa ajabu, na kuonekana kama kiumbe aliyeumbwa maalumu kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine, Mrefu alimwokoa Mwelekevu alipojitosa baharini (Robert, 1952). Urefu wa namna hiyo ni wa ajabu na ni muujiza kumpata mtu mrefu kiasi hicho katika maisha halisi. Hata hivyo, katika uhalisiajabu, kuwapata wahusika wa aina hiyo ni hali ya kawaida. Hii inashadidiwa na mhimili wa Nadharia ya Uhalisiajabu ulioelezwa hapo juu kuwa, katika uhalisiajabu, viumbe wa ajabuajabu wenye uwezo na nguvu kupindukia kama mazimwi, majitu, mizuka, mizimu pamoja na majini hurejelewa.

Urefu wa Mrefu unaakisi asili ya ujumbe alioubeba na kuutoa. Urefu wake unaashiria mawanda mapana ya ujumbe mtakatifu aliokuwa nao. Mrefu anafananishwa na nabii aliyetumwa na Mungu akiwa na ujumbe mtakatifu kwa ajili ya kuokoa wenye dhambi. Robert anasema kuwa Mrefu anaonekana kama kiumbe aliyeumbwa maalumu kuokoa kitu motoni, baharini au katika hatari nyingine. Kinachomsikitisha Robert ni kuwa, kwa sababu ya ibada ya kimizimu, ujumbe wa wokovu ulioletwa na Mrefu ulikataliwa.

Wafula (1989) anaeleza kuwa ujumbe wa Mrefu, kama unavyoelezwa na Robert, ulikuwa mzito ambao ni zaidi ya ujumbe unaoweza kutolewa na binadamu wa kawaida kwa wanadamu wenzake. Anaendelea kusema kuwa kukataa ujumbe wa Mrefu, ambao Robert aliamini kuwa ni kwa ajili ya uzima wa milele, kulimfanya awalinganishe watu wa mji wa Fahari (mji uliogeuzwa mawe) na wenye mioyo migumu kama mawe. Watu kama hao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao iliyo kama mawe, ni bubu na ni viziwi na, hivyo, kuhalalisha hali ya kutokuwa na uhai ndani mwao.

Mrefu, katika ujumbe wake, anasema kuwa mfalme ni mwakilishi wa Mungu duniani. Kwa hiyo, ufalme ni amana kubwa inayotaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa wanadamu. Hivyo, anasisitiza kuwa wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa mwadilifu katika matendo na maneno yake. Kila tendo, jema au baya, alitendalo ni mfano kwa raia wake. Mrefu anamwonya Tukufu kuwa uwezo usio hadhari ni kileo kibaya sana na ni vyema kufikiri kwa makini kabla ya kutoa jibu katika jambo lolote (Robert, 1952).

Robert, kwa kumtumia mhusika Mrefu na kisa cha mji uliogeuzwa mawe, ni dhahiri kuwa anazungumzia tawala mbalimbali za kijadi katika Bara la Afrika za wakati wake, jamii za Tanganyika zikiwamo. Tawala hizi zilikuwa bado zimekita imani zake katika ibada za kimizimu kiasi kwamba ilikuwa vigumu kuacha imani hizo. Hata hivyo, anasisitiza nguvu na uwezo wa imani ya Kikristo na Kiislamu kama suluhisho la kuwaondoa watu katika imani za kimizimu ambazo zinaonekana kama upuuzi mtupu. Anasema kuwa, ingawa wengi wanaweza kutaka kushikilia umizimu, lakini, kutokana na uwezo na athari za Ukristo na Uislamu, umizimu utashindwa milele. Hii ndiyo maana, Tukufu aliyewakilisha ibada ya kimizimu kwa kutojali onyo la Mrefu, alisababisha miji mingine yote ya dola yake kugharikishwa, na kila kiumbe aliyechokuwa na maisha katika mji wa Fahari kugeuka jiwe.

Robert anapotaka kuzungumzia siasa ya ukandamizaji na wizi wa mali ya Waafrika wakati wa serikali ya kikoloni, anawatumia wahusika majitu wenye nguvu na uwezo wa ajabu. Kwa mfano, katika, riwaya ya *Kusadikika*, anamtumia mhusika wa ajabu, Jeta, mfalme wa nchi ya Majuju. Anasema:

> Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepa kinywa hicho. Tani milioni moja za miamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo, na milioni nyingi za samaki zilimiminika pamoja na mkondo wa maji humo kinywani pia kila dakika tano. Lakini kila dakika moja Jeta alilia: kiu njaa, kiu njaa (Robert, 1951:23).

Kitendo cha mtu kupanua mdomo na maji ya mto mkubwa, tani za chuma, magogo na samaki kumiminika kinywani na kuendelea kulia muda huohuo ‘kiu njaa, kiu njaa’ ni hali isiyo ya kawaida na ni muujiza kumpata mtu kama huyo katika ulimwengu wa kawaida.

Kiwango cha ulaji na aina ya vyakula anavyokula Jeta hakielezeki kwa kutumia nadharia za kisayansi wala za kihalisia bali kwa kutumia Uhalisiajabu. Maelezo hayo yanashadidiwa na mhimili wa uhalisiajabu unaodai kuwa uhalisiajabu unatoa kipaumbele kwa mazingira na viumbe wa ajabuajabu kama mazimwi, mashetani, mizuka, majitu pamoja na majini kwa kupeleka hadhira katika safari ya hali na matukio ya kweli na yanayowezekana. Mhimili huo umetuwezesha kuchunguza ulafi wa Jeta kama kisa cha kawaida kinachowakilisha matukio ya kweli katika mazingira halisi katika jamii husika. Zamora (2005) anakubaliana na mawazo hayo kwa kusema kuwa, kwa ujumla, uhalisiajabu hutambulishwa kwa sifa yake ya kuunda maana ya kimazingaombwe kwa kuangalia vitu vya kawaida kwa namna isiyo ya kawaida.

Shaaban Robert ametumia ulafi na uroho wa Jeta ili kuelezea matendo ya viongozi waroho, walafi, wenye tamaa na wasiotosheka. Hawa viongozi hawaridhiki hata kama watachukua mali yote ya nchi kwa faida yao binafsi. Mwandishi anasema:

> Mfalme alitaka kumla Kabuli bila kugawana na wawinda waliomkamata. Choyo chake kikubwa kiliwaudhi wawinda, pakatokea vita kati ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo kila kitu kilichokuwa na uhai kiliangamizwa (Robert, 1951:23).

Shaaban Robert, kwa kutumia mhusika wa ajabu, Mfalme Jeta, alikusudia pia kuisema serikali ya kikoloni iliyokuwa inasomba mali na kila kitu kilichokuwa kinapatikana Afrika bila kutosheka. Licha ya serikali ya kikoloni kusomba kila kitu kutoka Afrika, lakini haikushiba, haikutosheka wala kuridhika. Kila dakika moja, baada ya kumeza tani zote hizo, Jeta analia kiu njaa, kiu njaa (Robert, 1951).

Kezilahabi, kwa namna inayokaribiana na Robert, anatumia maelezo ya msimuliaji, maneno ya wahusika na matendo yao kuwatambulisha wahusika majitu wenye nguvu na uwezo wa ajabu. Wahusika wa aina hiyo wanaotumiwa na Kezilahabi ni Mtume, Mfuasi na Mtenzi ambao wana matendo yanayotaka kufanana.

Mtume anaweza kuongea na malaika (Gabrieli), ana nguvu za ajabu na, kwa nguvu hizo, anabeba mlima uliokuwa unawazuia kuziona nyayo za Paa na kuutupa pembeni (Kezilahabi, 1990). Pia, miujiza ya mhusika huyu inadhihirika zaidi alipousukuma kando mlima uliokuwa unamzuia mfalme kupata mwanga wa jua la asubuhi. Mwandishi anasema:

> Tulipoufikia mlima mtume alifumba macho. Kwa nguvu kabisa aliusukuma mlima kwa bega. Mlima ulianza kusukumika polepole hadi ulipotoa nafasi ya kutosha (Kezilahabi, 1990:32).

Kitendo cha binadamu kusukuma mlima si cha kawaida na kinamshangaza hata mfalme aliyetoa agizo la kusukuma mlima kama mtihani mmojawapo wa kumpata Paa. Hii inajidhihirisha kwa namna alivyowatazama wasaka Paa kwa mshangao alipowaita kuwapa mtihani wa tatu (Kezilahabi, 1990).

Mhusika mwingine kama jitu lenye uwezo wa ajabu ni Mfuasi. Jina la Mfuasi linalotokana na kitenzi fuata. Kufuata ni kitendo cha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa makusudi maalumu. Mfuasi ni mhusika wa ajabu kwa sababu ananyoosha mguu wake mrefu na kufuata kiko cha mfalme alichokisahau Sibara umbali wa safari ya miaka saba (Kezilahabi, 1990). Mguu wake ni mrefu kiasi cha

kutoonekana ulikoishia na anapoukunja unatengeneza njia ya kufuatwa na wasaka Paa. Mfuasi anasema Paa anayetafutwa alipita juu ya mguu wake. Kwa hiyo mguu wake ni njia inayofuatwa na watu wenye azma maalumu ya kutafuta kitu fulani. Msimuliaji anamwelezea hivi:

> Miguu yake haikuwa inalingana. Mguu mmoja ulikuwa mfupi na mwingine mrefu sana. Hatukuweza kuona ulikoishia. Huo mguu ndio utakaokuelekeza uendako. Huu ndio mguu uendao mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo. Paa mmtafutaye alipita juu ya mguu huu. Mfuasi alianza kuukunja ule mguu mrefu hadi ulipokuwa sawa na mwingine (Kezilahabi, 1990:28).

Mtu mwenye mguu mrefu ambao hauwezi kuuona ulikoishia kwa sababu ya urefu wake na unaoweza kukunjwa na kuwa sawa tena na mguu mwingine ni muujiza kuonekana duniani. Uajabu wa mhusika huyu unajidhihirisha zaidi pale wanapotumwa kufuata kiko cha mfalme alichokisahau Sibara umbali wa mwendo wa miaka saba. Mfuasi anaukunjua mguu wake. Mara baada ya kuukunjua, kwa muda mfupi ukawa umesafiri umbali wa mwendo wa miaka saba. Pia, anapoukunja mguu unarudi na kiko cha mfalme (Kezilahabi, 1951). Huyu ni mhusika wa ajabu. Si rahisi katika uhalisia mguu wa binadamu kukunjuka, kuwa mrefu na kusafiri kilomita nyingi kwa kasi kiasi hicho kwa kukunjuliwa tu. Zaidi ya yote, mguu wa Mfuasi ni wa ajabu zaidi kwa sababu unawaelekeza watu njia na una uwezo wa kwenda mbali kwenye fikra na uzamapo haurudi bila wazo (Kezilahabi, 1990).

Mguu wa Mfuasi unahimiza kufikiri, kuwa ukizama katika kuwaza hautoki bure bali lazima utoke na wazo. Maoni hayo ni sawa na mawazo ya Plato aliyewahi kusema kuwa, ili binadamu aweze kuishi maisha yenye maana, ni lazima ajifunze kufikiri na katika kufikiri ndipo atakapofahamu ukweli kama ulivyo na lengo la kuwapo kwa kila kitu duniani (Mihanjo, 2006). Kwa maana hiyo, inawezekana Kezilahabi ametumia jina la Mfuasi kusisitiza umuhimu wa kufikiri; kwamba, ili kuupata kweli, ni lazima kufikiri. Amelinganisha fikra na safari ndefu isiyo na mwisho (urefu wa mguu wa Mfuasi). Hata hivyo, mtu yeyote atakayezama katika kuwaza na kufikiri kwa makini, hatatoka bure. Ni lazima atoke na wazo au jambo fulani la maana na lenye faida kwa jamii. Hilo atakalolipata ndilo kweli.

Mtenzi, kama mhusika jitu lenye uwezo wa ajabu, anajieleza hivi:

> Mimi naitwa Mtenzi. Mimi ndiye mkausha maji. Mfuasi wa mwisho. Mtenzi aliinama akanywa maji yote yaliyokuwa mtoni (Kezilahabi, 1990:28).

Ni muujiza binadamu wa kawaida kunywa maji yote ya mto; tena mara moja. Hii inadhihirisha kuwa Mtenzi ni mhusika wa ajabu. Uajabu wa Mtenzi unajidhihirisha zaidi pale wanapopewa kulima robo ekari ya shamba kavu katika ardhi ngumu ambapo jembe haliwezi kuingia hata robo inchi. Mtenzi alitapika maji aliyokunywa mtoni na kulowesha shamba lote na ardhi kuweza kulimika (Kezilahabi, 1990). Hali isiyo ya kawaida ya Mtenzi inazidi kuonekana walipokuwa wakitoka katika safari ya kumsaka Paa. Alipofika pale wenzake walipomkuta, alitapika maji yakajaa mto na kubaki akiyatazama maji hayo (Kezilahabi, 1990). Hii inazidi kubainisha kuwa Kezilahabi ametumia wahusika majitu wenye uwezo wa ajabu katika riwaya zake teule. Khamis (2007) anakubaliana na wazo hili kwa kusema kuwa Kezilahabi amewapa wahusika wake nguvu za kichawi na kimiujiza. Wanaweza kuhamisha milima na kumeza maji yote ya mto na kuyatema tena na kunyoosha miguu kwa maelfu ya maili kuchukua kitu.

Wahusika hawa ni muujiza kuwakuta katika mazingira halisi. Hii ni kwa sababu ni muujiza kwa binadamu wa kawaida kunywa maji yote ya mto, kutapika maji yanayoweza kulowanisha shamba au kutapika maji yakajaa mto, kubeba na kuhamisha mlima au kukunjua mguu ukaenda umbali wa maili nyingi. Hata hivyo, matendo na maelezo ya wahusika hao, yakichunguzwa, bado yanasadifu tu mawazo ya Kezilahabi kuwa katika kufikiri kunapatikana ufumbuzi wa matatizo yote. Kwa sababu ya fikra makini, binadamu ametengeneza mashine zinazopasua milima ili kutengeneza barabara. Kwa fikra hizo, binadamu ametengeneza mabomu ya kuvuna mvua angani bila kusubiri mvua za misimu. Pia, kwa kufikiri, binadamu amefanikiwa kufanya ulimwengu kuwa kama kiganja cha mkono na, hivyo, kuweza kuzunguka au kuona yote yanayotendeka duniani kwa dakika moja.

### 4.3 Wahusika Wenye Uwezo wa Kusoma Mawazo ya Mtu

Aina nyingine ya wahusika wa ajabuajabu ambao wanabainishwa kutokana na matendo yao pamoja na maelezo ya mwandishi (msimuliaji) ni wahusika wenye uwezo wa kusoma na kufahamu mawazo ya mtu. Hawa wahusika wanaweza kufahamu mtu anafikiri nini na pia kufahamu mambo yanayotendeka katika mazingira mengine yaliyo mbali nao.

Ili kubainisha aina hii ya wahusika, tumetumia mhimili wa Uhalisiajabu unaosema kuwa, katika uhalisiajabu, kaida za kimazingira na mahali huvunjwa. Hivyo, mtu anaweza kuingia popote hata ndani ya ardhi bila kizuizi, kufahamu yanayotendeka mbali na kufahamu mawazo ya mtu pamoja na kuzungumza na viumbe wengine bila kizuizi cha tofauti ya lugha.

Shaaban Robert anamtumia Huria kubainisha aina hii ya wahusika. Huria ana uwezo wa kufahamu jambo linalotendeka mbali katika mazingira mengine tofauti. Alifahamu kuwa Adili ametoswa baharini na ndugu zake na pia alifahamu kuwa Adili hakuwaadhibu manyani, yaani Hasidi na Mwivu, lakini hakuwapo katika mazingira hayo (Robert, 1952).

Kezilahabi, kwa upande wake, anamtumia Paa kama mhusika mwenye uwezo wa kufahamu mawazo ya mtu. Paa anapojibadilisha kuwa msichana, anakuwa na uwezo wa kumsoma mtu na kufahamu anayoyawaza. Mwandishi anasema:

> Sasa tulikuwa wawili tu. Mimi mwindaji na Paa. Nilianza kujiuliza moyoni, “Huyu msichana ni nani kwangu, na mimi ni nani kwake.” Alisimama. Alinitazama, akatabasamu. “Najua” alisema. Unafikiri msichana ni nani kwa mvulana ambaye ameingia katika duara yake?”. Nilianza kujiona mtu mzima tayari kushika madaraka na majukumu, “Je nimekua?” nilijiuliza kimoyomoyo. Aligeuka tena. “Najua umekua. Lakini haitakuwa! Labda siku ya ngoma kuu, nitakapokukalia mabegani na kubana shingo lako kwa mapaja yangu” (Kezilahabi, 1990:36).

Kitendo cha ajabu kisicho cha kawaida cha Huria na Paa kufahamu mawazo ya mtu na mambo yanayotendeka katika mazingira mengine mbali na pale walipo si cha kawaida katika maisha halisi. Hali hiyo haiwezi kuelezwa kwa kutumia nadharia za kihalisia wala kuthibitishwa kisayansi bali kwa kutumia Nadharia ya Uhalisiajabu. Hii inathibitishwa na mhimili wa uhalisiajabu uliofafanuliwa hapo juu kuwa, katika uhalisiajabu, mipaka yote huvunjwa. Hivyo, hakuna mpaka kati ya mtu na mtu, jamii na jamii, nchi na nchi, mbali na karibu. Kaida za uasilia na za uhalisia huvunjwa; hivyo, binadamu anaweza kuona na kufahamu mambo yanayotendeka katika mazingira yaliyo mbali na kufahamu anayoyawaza mtu mwingine (Roh, 1925).

### 4.4 Wahusika Hai-Wafu

Wahusika hai-wafu ni aina ya wahusika wanaoishi kati ya uhai na kifo, yaani wanakufa na kuwa hai kwa wakati mmoja. Katika jamii nyingi za Kiafrika, watu waliokufa karibuni wanahesabika kama watu walio katikati ya uhai na kifo. Hivyo, wanaitwa hai-wafu (Mbiti, 2011). Hai-wafu wanaweza kurudi na kushirikiana na familia zao katika shughuli mbalimbali kimiujiza. Hata hivyo, walio hai wanaogopa kukutana nao kwa sababu wanaamini kuwa watu hao wamekufa. Kwa hiyo, kukutana nao ni tukio la ajabu na ni uvunjivu wa kaida kati ya uhai na kifo.

Ili kubainisha wahusika hai-wafu, tumetumia mhimili wa Uhalisiajabu unaosema kuwa uhalisiajabu unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya ukweli na

uongo, ndoto na urazini, uhai na kifo, sasa na zamani, utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kezilahabi anatumia maneno ya wahusika, matendo yao na maelezo ya msimuliaji kuwabainisha wahusika hai-wafu. Kwa mfano, anamtumia mhusika Nabii anayejieleza hivi:

> Walinifikiria kichaa, wale ambao hawakuniamini. Vichaa, wazinzi na maskini ndio waliokuwa wa kwanza kunizunguka na kunifuata. Waliniua mimi badala ya kuua Sphinx (Kezilahabi, 1990: 26).

Maelezo ya Nabii yanayomhusu binafsi yanaonesha kuwa ni mhusika wa ajabu. Hii ni kwa sababu anasema kuwa aliuawa badala ya Sphinx, yaani alikufa lakini bado anaongea na walio hai. Kwa hiyo, ni mhusika mfu na wakati huohuo anaishi. Kufa au kuuawa ni jambo la kawaida linalotokea kila siku katika maisha ya wanadamu. La ajabu, katika maelezo ya Nabii, ni maneno yake. Nabii anasema aliuawa badala ya Sphinx. Hakuna binadamu anayeweza kufa na kuishi kwa wakati huohuo, yaani Nabii aliuawa lakini bado anaweza kuzungumza tena na walio hai na kueleza yeye mwenyewe kuwa aliuawa badala ya Sphinx. Hata hivyo, katika uhalisiajabu, kuna uwezekano mkubwa wa mtu kufa na kuishi kwa wakati mmoja. Uwezekano huo unathibitishwa na mhimili wa uhalisiajabu uliouelezwa hapo juu ambao unadai kuwa, katika uhalisiajabu, hakuna mpaka kati ya uhalisi na utohalisi. Hii ni kwa sababu uhalisiajabu haukubaliani na uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali kama za uhalisi na ndoto, usasa na ukale, uhai na kifo, mbali na karibu, ugeni na uenyeji na tamaduni zinaingiliana.

Flores (1998) anafafanua mhimili huo wa uhalisiajabu kwa kusema kwamba uhalisiajabu unajumuisha uchanganyaji wa uhalisia na fantasia. Unakusudia kuunganisha na kuvunja mpaka kati ya ukweli na uongo, ndoto na urazini, uhai na kifo, sasa na zamani, utoto na utu uzima na mbali na karibu. Kwa maana hiyo, lengo la uhalisiajabu katika fasihi ni msisitizo wa umoja kati ya mazingaombwe na uhalisia.

Maelezo ya Nabii yanasisitiza utata wa Kezilahabi juu ya maisha baada ya kifo. Hii inatokana na imani mbalimbali miongoni mwa jamii za Kiafrika juu ya maisha baada ya kifo. Kuna wanaoamini kuwa wafu wanarudi kuishi miongoni mwao kupitia: jina lake kutajwa mara kwa mara, kuzaliwa upya katika ukoo wake au kwa jina lake kuendelezwa kwa watoto wanaozaliwa kuitwa kwa jina lake (Mbiti, 2011). Waafrika wanaamini kuwa marehemu/maiti bado ni mtu. Wengine wanaamini kuwa, baada ya kufa, wafu hurudi kuishi na kushirikiana na jamii zao katika shughuli mbalimbali ingawa hawaonekani kwa macho (Scott, 2010; Mbiti, 2011).

### 4.5 Wahusika wenye Kuvunja Kaida za Kimawasiliano kati ya Binadamu na Viumbe Wengine

Mawasiliano ni kupashana habari au kubadilishana ujumbe baina ya wawasilianaji, kwa mfano, mtu na mtu au mtu na kikundi cha watu. Viumbe wengine kama wanyama nao huwasiliana ingawa mawasiliano yao yanahusisha ishara na sauti tofauti na binadamu ambaye hutumia lugha katika mawasiliano (Mdee, Njogu na Shafi, 2011). Lugha ya binadamu, tofauti na mawasiliano ya wanyama, inajitokeza katika viwango viwili, sauti na maana. Viwango hivyo huunganishwa ili kupata neno lenye maana tofauti, kwa mfano, fonimu, maneno na sentensi. Kinyume chake, mawasiliano ya wanyama hayawezi kuchanganuliwa kwa kuanzia kipashio kidogo hadi kikubwa. Hii ni kwa sababu namna ya mawasiliano yanayotumia lugha ya kutamkwa hutumiwa na binadamu pekee (Massamba, 1999). Kwa hiyo, inapotokea wanyama na viumbe wengine kama majini, malaika na ndege wakatumia lugha ya kutamkwa na kuwasiliana na wanadamu kwa kutumia lugha bila utata wowote, hapo ndipo inaposemwa kuwa wahusika hao ni wa ajabu. Faida kubwa ya kutumia njia hii katika kazi za fasihi ni kuwa mwandishi anaweza kumtumia mhusika kufanya lolote atakalo na kuwasiliana na mtu au kiumbe mwingine yeyote bila pingamizi lolote.

Ili kuwabainisha wahusika wenye kuvunja kaida za kimawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine, tumetumia mhimili wa Uhalisiajabu unaodai kuwa, katika uhalisiajabu, kaida za kimazingira na mahali huvunjwa. Hivyo, mtu anaweza kuingia popote hata ndani ya ardhi bila kizuizi, kufahamu yanayotendeka mbali, kufahamu mawazo ya mtu, pamoja na kuzungumza na viumbe wengine bila kizuizi cha tofauti ya lugha.

Robert na Kezilahabi wametumia maneno ya wahusika wenyewe na maelezo ya mwandishi kutambulisha aina hii ya wahusika. Robert, kwa mfano, anamtumia Ridhaa kuwasiliana na viumbe wa kufikirika kama malaika na shetani. Ridhaa, mjumbe wa mbinguni, baada ya kufika mbinguni kwa msaada wa malaika, anafanikiwa kuleta ujumbe wa mambo ya mbinguni nchini Kusadikika. Pia, shetani anafanikiwa kunyemelea halmashauri mbili za mbinguni na kufanikiwa kueneza umbea wa siri za mbinguni nchini Kusadikika.

Shetani kuzungumza na wanadamu na kuwaletea umbea au uongo wa siri za mbinguni ni suala la kuwazika ambalo haliaminiki katika uhalisia wa maisha ya kawaida na ya kila siku. Hata hivyo, kwa kuwatumia wahusika wanaovunja kaida za kimawasiliano, kuwasiliana na kutagusana kati ya binadamu na malaika, mashetani, majini na hata wafu, ni suala la kawaida. Licha ya lugha ya malaika na ya mbinguni kutojulikana kwa wanadamu katika hali halisi, lakini Ridhaa, mjumbe wa mbinguni, anafanikiwa

kusikiliza na kuzungumza na malaika na kuleta habari za mbinguni nchini Kusadikika (Robert, 1951).

Kezilahabi anawatumia Simba na Pundamilia kuvunja kaida za kimawasiliano kati ya wanadamu na wanyama. Anasema kuwa Msimuliaji pamoja na mwenzake (mkewe) walipowaona watoto wawili wanaong'ara kama wao juu ya mlima, waliamua kwenda kuwaona, ndipo pundamilia na simba walipojitolea kuwapeleka. Mwandishi anasema:

> "Nitakupeleka," Pundamilia alisema. "Na mimi nitakupeleka," Simba alimwambia mwenzangu. "Na tufanye mashindano, tuone nani atafika kwanza pale kileleni," pundamilia alitoa wazo. Tulipanda juu ya migongo yao, na mara walianza kukimbia kuelekea kileleni (Kezilahabi, 1991).

Si suala la kawaida na halitarajiwi katika uhalisia wanyama kama pundamilia na simba kuwasiliana na wanadamu kwa kutumia lugha ya kutamkwa ambayo hutumiwa na wanadamu tu kuwasiliana miongoni mwao. Wanyama kutumia lugha ya kutamkwa ni tukio la ajabu na la kuogofya, na ni uvunjivu wa kaida za mawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine. Pinker (1994) anashadidia hili anapozungumzia utabaka wa lugha kwa kusema kwamba mfumo wa mawasiliano ya viumbe wasio wanadamu yana muundo wa aina tatu: milio yenye ukomo, ishara za kianalojia zenye kuendelea ambazo zinaonesha namna hali ilivyo au seti isiyo na utaratibu ya mabadiliko ya mada. Mfumo huo ni tofauti na lugha ya binadamu ambayo ina muundo tofauti kabisa ambapo tabia ya mfumo wa muungano uitwao sarufi huifanya kuwa iso ukomo, yenye kuherufika na kutungika. Hata hivyo, kwa wahusika wa ajabuajabu, ni hali ya kawaida kuvunja kaida za mawasiliano kati ya binadamu na viumbe wengine. Hivyo, binadamu anaweza kuongea na simba, pundamilia, majini na hata miti kwa kutumia lugha ya kutamkwa bila kizuizi chochote. Walibora (2010) anasisitiza anaposema kwamba Uhalisiajabu unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama nadharia inayowakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imesawiri aina mbalimbali za wahusika wa ajabuajabu katika riwaya teule za Robert na za Kezilahabi. Imedhihirika kuwa wote, Robert na Kezilahabi, wametumia aina za wahusika wa ajabuajabu kwa namna zinazofanana na kwa namna tofauti katika riwaya zao teule. Robert amewatumia wahusika wa ajabuajabu kuelezea umuhimu wa kutenda mema na kusisitiza kuwa kila mmoja hulipwa kadiri ya matendo yake. Anasisitiza mabadiliko kwa kuhimiza jamii kuwapa wanawake uhuru wa kuchagua mustakabali wa maisha yao na kuachana na ukale usio na faida kama vile ibada ya kimizimu. Kezilahabi, kwa upande wake, ametumia aina za wahusika wa

ajabuajabu kujaribu kueleza umuhimu wa kufikiri. Pia, amewatumia wahusika hao kujaribu kufumbua fumbo la maisha baada ya kifo, suala ambalo bado limekuwa kitendawili ambacho kimeshindikana kutegulika. Hata hivyo, anahimiza kuwa, ili kutegua kitendawili hicho, kinachotakiwa ni kufikiri.

**Marejeleo**

Abrams, M.H. (1999) *A Glossary of Literary Terms* (7th ed.). Boston: Heinle & Heinle.

Bosibori, B.T. (2016) *Mwingiliano Matini Katika Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi

Bowers, M.A. (2004) *Magical Realism*. New York: Routledge.

D'Haen, T.L. (2005) "Magical Realism and Postmodernism". Decentering Priviledged Centers." Katika Zamora, L. P. na Faris, W.B. (Wah.) *Magical Realism: Theory, History, Community*, Durban na London: Duke University Press. PP. 191-208.

Flores, A. (1988) "Magical Realism Strategies". Katika Scott, S. (Mh.) *The Suppliment of Realism: Twentieth Century Literature*. Durham: Duke University Press. Juz. 34(2):140-154.

Green, M.J.A. (2009) Dreams of Freedom: Magical Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake. *Romanticism*, Juz. 15(1):18-32.

Kezilahabi, E. (1990) *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991) *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S. (2007) "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili". *Kioo cha Lugha*. Juz. 513-23

Leal, L. (2009) *Magical Realism in Spanish American* Literature. Katika Zamora, L. P. na Faris, W.B. (Wah.) *Magical Realism: Theory, History, Community*. Durban na London: Duke University Press. (PP. 119-124).

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printers and Stationary.

Maggati, C.N (2022) *Uchawi na Mazingaombwe katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Massamba, D.P.B. (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbiti, J.S. (2011) *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Mdee, J.S., Njogu, K. na Shafi, A. (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*. Dar es Salaam Tanzania: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Mihanjo, A. (2006) *Falsafa na Usanifu wa Hoja-Kutoka Wayunani Hadi Watanzania* (Waafrika). Morogor: Salvatorianum Publishers.

Mpalanzi, L. (2018) "Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi Kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili". *Mulika*. Juz. 37(1):131-143

Mturo, N.J. (2018) *Jiniuchawi na Ushirikina kama Mkakati wa Uchimuzi Katika Riwaya Teule za Maundu Mwingizi*.Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Onchwati, S. J. (2016) *Uhalisiajabu Unavyojitokeza katika Ukawafi wa Miraji na Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Osore, M.K. (2008) *Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Pinker, S. (1994) *The Language Instict: How the Mind Creates Language*. New York: William Morrow and Company

Robert, S. (1951) *Kusadikika*. Nairobi: Evans Brothers, Kenya Ltd.

Robert, S. (1952) *Adili na Nduguze*. London and Basingstone: Macmillan Publishers.

Roh, F. (1925) *Magic Realism: Post–Expressionism. Magical Realism:Problems of the Newest European Painting.* Leipzig Germany:Klinkhardt & Biermann.

Rono, P. (2013) *Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa Kidagaa Kimemwozea*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Salim, M.A. (2015) *Kuchunguza Ufasihi Simulizi Unaojitokeza Ndani ya Hadithi za Kusadikika na Adili na Nduguze*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Senkoro, F.E.M.K. (2011) *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Scott, R.M. (2010) *Birth Death and Feminity: Philosophes of Embodiment*. Bloomington: Indiana University Press.

Schroeder, S. (2004) *Rediscovering Magic Realism in the Americas*. West Port: Praeger.

Wafula, R. (1989) *The Use of Allegory in Shaaban Robert's Prose Works*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Walibora, K. (2010) "Uhalisiamazingaombwe. Mshabaha kati ya Dunia Yao na the Tin Drum". *Swahili Forum*, Juz. Na. 17: 143-157.

Wamitila, K. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Book.

Wamitila, K. (2008) *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. (2010) *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Warner, C. (2006) Magic Realism and German Idealism. *Modern Language Review*, Juz. Na. 101/2: 488-498.

Zamora, P.L. na Faris, B.W. (1995) *Magical Realism Theory, History Community*. London: Duke University Press.